**HOTUBA YA BALOZI MHANDISI JOHN W.H. KIJAZI,
KATIBU MKUU KIONGOZI, WAKATI WA UFUNGUZI WA
MAADHIMISHO YA SIKU YA WAHANDISI KWA MWAKA 2017,
UKUMBI WA JAKAYA KIKWETE, DODOMA,
SEPTEMBA 7, 2017**

---

***Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano,
Prof. Makame M. Mbarawa (Mb.);***

***Waheshimiwa Mawaziri na Wabunge wote mliohudhuria;***

***Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa wa Dodoma,
Bwana Jordan Rugimbana;***

***Katibu Mkuu (Ujenzi),
Mhandisi Joseph M. Nyamhanga;***

***Makatibu Wakuu wote mliohudhuria;***

***Mwenyekiti wa Bodi ya Usajili wa Wahandisi,
Mhandisi Prof. Ninatubu Lema;***

***Wenyeviti wa Bodi nyingine mbalimbali mliopo;***

***Wajumbe wa Bodi ya Usajili wa Wahandisi;***

***Mhandisi Patrick Barozi,
Kaimu Msajili wa Bodi ya Usajili wa Wahandisi;***

***Rais wa Bodi ya Wahandisi ya Misri (Egyptian Syndicate of Engineers)
pamoja Wasajili wa Bodi za Wahandisi kutoka Kenya,
Uganda na Rwanda;***

***Wakuu wa Taasisi mbalimbali na wadau wa
Sekta ya Ujenzi na Taaluma ya Uhandisi;***

***Washiriki Wote wa Mkutano huu;***

***Wanahabari;***

***Wageni Waalikwa;***

***Mabibi na Mabwana.***

**Habari za Asubuhi!**

Napenda nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kutujalia afya njema na kutuwezesha kukutana leo kwa ajili ya kuadhimisha Siku hii ya Wahandisi Tanzania kwa mwaka huu wa 2017.

Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi, nachukua fursa hii pia kukushukuru wewe binafsi, Wizara yako pamoja na Bodi ya Usajili wa Wahandisi kwa mwaliko mliotoa kwa Mheshimiwa Rais, kuja kuzungumza na Jumuiya hii ya Wahandisi na Washiriki wengine katika maadhimisho haya ya Siku ya Wahandisi Tanzania kwa mwaka 2017.

Aidha, kipekee kabisa namshukuru sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, **Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli** kwa kunipa heshima ya kumuwakilisha katika maadhimisho haya muhimu. Mheshimiwa Rais angependa sana kushiriki pamoja nasi katika maadhimisho haya, lakini kutokana na majukumu mengine ya kitaifa yanayomkabili, hakuweza kufanya hivyo. Pamoja na udhuru huo, Mheshimiwa Rais amenituma niwapongeze sana kwa kuandaa na kufanikisha maadhimisho haya, na anawatakia Siku ya Wahandisi yenye mafanikio.

Kipekee nawapongeza wote walioshiriki katika maandalizi ya Mkutano huu ambao nimejulishwa kuwa umehudhuriwa na wahandisi takriban 2,000 wa fani mbalimbali kutoka ndani na nje ya nchi yetu. Vilevile, nimejulishwa kuwa miongoni mwa washiriki kutoka nje ya nchi, wapo ambao ni mara yao ya kwanza kufika Mjini Dodoma. Hivyo nachukua fursa hii kuwakaribisha hapa Dodoma, Makao Makuu ya Nchi na Serikali. Karibuni sana na mjisikie mko nyumbani.

**Ndugu Wajumbe wa Mkutano:**

Kama inavyofahamika, lengo la siku hii ya Wahandisi ni kutoa nafasi ya kipekee kwa Wahandisi na wadau wengine wa fani hii ili (i) kukutana na kujadili masuala mbalimbali kuhusu taaluma ya uhandisi; (ii) kufanya maonesho ya kiufundi na kibiashara yanayoonesha ubunifu wa kihandisi; (iii) kuwatambua na kuwazawadia **wahandisi wahitimu** (*Graduate Engineers*) waliofanya vizuri katika mafunzo yao; na (iv) kuwaapisha wahandisi waliokidhi vigezo.

Nimejulishwa kuwa majadiliano katika Mkutano huu wa siku mbili yatajikita katika mada kuu isemayo: **"Jukumu la Sayansi, Teknolojia, Uhandisi na Hisabati katika Kukuza Viwanda kwa Maendeleo ya Kijamii na Kiuchumi."** Aidha, washiriki wa Mkutano watapata fursa ya kusikia mada **sita** tofauti zitakazowasilishwa na viongozi mbalimbali waandamizi wa Serikali na Taasisi za Umma ambao watasisitiza umuhimu wa Sayansi, Teknolojia, Uhandisi na Hisabati (*Science, Technology, Engineering and Mathematics* - **STEM**) katika kukuza sekta ya viwanda, kwa maendeleo ya kijamii na kiuchumi. Ni matumaini yangu kuwa mada hizo zitasaidia kutoa mwelekeo makini na sahihi wa jinsi ya kutumia taaluma ya uhandisi kwa kushirikiana na taaluma nyingine katika kujenga uchumi wetu wa Tanzania ya Viwanda.

Naipongeza sana Wizara pamoja Bodi ya Usajili wa Wahandisi kwa kuchagua mada hii ambayo inaakisi azma ya Serikali ya Awamu ya Tano ya kujenga uchumi wa viwanda na kuzipatia ufumbuzi changamoto za msingi kwa maisha ya Watanzania, hususan walio maskini. Ni dhahiri kuwa Wahandisi tunao mchango mkubwa na muhimu katika ufanikishaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2016/17-2020/21) ambao tumeanza kuutekeleza tangu mwezi Julai, 2016.

**Ndugu Wajumbe wa Mkutano, Mabibi na Mabwana:**

Tanzania, kama zilivyo nchi nyingine duniani, inategemea Wanasayansi kubuni mbinu za kukabiliana na changamoto mbalimbali za kimaendeleo, ikiwa ni pamoja na athari za mabadiliko ya tabianchi; uchafuzi wa mazingira; upatikanaji wa maji safi na salama; upatikanaji wa miundombinu mbalimbali ikiwemo ya usafirishaji na nishati ya bei nafuu; na kupambana na maadui wakubwa wa taifa yaani maradhi, ujinga na umaskini. Hata hivyo, takwimu zinaonesha kuwa idadi ya Wanasayansi, wakimemo Wahandisi katika nchi zinazoendelea, Tanzania ikiwemo, haikidhi mahitaji ya wataalam wa fani hiyo. Kwa mujibu wa takwimu za Bodi ya Usajili wa Wahandisi, hadi kufikia mwezi Juni, 2017 jumla ya Wahandisi 19,164 walikuwa wamesajiliwa katika ngazi mbalimbali. Miongoni mwa Wahandisi hawa, 17,451 ni Watanzania na 1,713 ni wageni.

Kwa kutambua mahitaji hayo, hususan katika kipindi hiki ambapo Tanzania imedhamiria kujenga uchumi wa viwanda na kuzipatia ufumbuzi changamoto za huduma za Kiuchumi na

Kijamii, Serikali inafanya jitihada za kipekee ili kuongeza idadi ya Wahandisi nchini. Jitihada hizo ni pamoja na zifuatazo:

(i) Kuboresha elimu ya sekondari na kuhamasisha vijana kusoma masomo ya Sayansi. Katika ufanikishaji wa suala hili msisitizo unawekwa kwa shule za sekondari kuwa na maabara bora za sayansi, walimu bora wa masomo ya sayansi, na vitabu vya sayansi vya kutosha;
(ii) Kuongeza nafasi za masomo ya Uhandisi katika vyuo vikuu;
(iii) Kuzishawishi shule na vyuo binafsi kufundisha masomo ya sayansi;
(iv) Kuongeza idadi ya Wasichana wanaosoma Uhandisi katika vyuo vikuu na vyuo vya mafunzo ya ufundi; na
(v) Kuongeza mafunzo kwa vitendo kwa Wahandisi Wahitimu (*Structured Engineers Apprenticeship Programme* - SEAP).

Ni dhahiri kuwa, kufanikiwa kwa jitihada hizi kutaiwezesha nchi kuwa na rasilimali watu ya kutosha katika fani za Uhandisi, Sayansi, Hisabati na Teknolojia kwa ajili ya kufanikisha ujenzi, ustawi na maendeleo ya viwanda pamoja na miundombinu yake. Vilevile kupitia jitihada hizi nchi itaweza kuwa na nguvukazi ya kutosha ambayo imeandaliwa vizuri kitaaluma, kiujuzi na kiuweledi katika ngazi zote (Wahandisi, Mafundi Sanifu na Mafundi Mchundo), ili kutekeleza majukumu yake kwa ubora na ufanisi unaotakiwa. Tunatarajia kuwa nguvukazi iliyoandaliwa vyema italeta matokeo chanya kwani itakuwa na ubunifu, uzalendo na uwezo wa kuhimili ushindani kutoka ndani na nje ya nchi yetu, na hivyo kuweza kushiriki kikamilifu katika utekelezaji wa miradi mikubwa ya kimkakati, ikiwemo ile iliyoainishwa katika Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano.

**Ndugu Wajumbe wa Mkutano, Mabibi na Mabwana;**

Chini ya Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano, ipo miradi kadhaa ambayo inatoa fursa kwa Wahandisi wa fani mbalimbali kushiriki. Miradi hiyo ni pamoja na:

(i) Mradi wa Makaa ya Mawe Mchuchuma;
(ii) Mradi wa Chuma Liganga;

(iii) Maeneo Maalum ya Uwekezaji (*Special Economic Zones* – SEZ);
(iv) Kituo cha Biashara na Huduma Kurasini;
(v) Ujenzi wa Reli ya Kati na Matawi yake kwa kiwango cha Kimataifa (*Standard Gauge*);
(vi) Mji wa Kilimo Mkulazi;
(vii) Ufufuaji wa Shirika la Ndege la Taifa.

Miradi mingine yenye kutoa fursa mbalimbali kwa Wahandisi, Mafundi Sanifu na Mafundi Mchundo ni katika ujenzi wa miradi mikubwa ifuatayo:

(i) Bwawa kwa ajili ya uzalishaji Umeme wa 2100 MW katika Bonde la Mto Rufiji (Stiegler's Gorge);
(ii) Bandari za Tanga, Dar es Salaam na Mtwara;
(iii) Bomba la mafuta ghafi kutoka Hoima (Uganda) hadi Bandari ya Tanga (Tanzania);
(iv) Bomba la kusafirisha maji kutoka Ziwa Victoria hadi miji ya Tabora, Nzega na Igunga, pamoja na miradi mingine ya ujenzi wa miundombinu mbalimbali ya maji;
(v) Barabara za juu kwenye makutano ya TAZARA (TAZARA Flyover) na Ubungo (Ubungo Interchange);
(vi) Miundombinu ya Mabasi Yaendayo Haraka (BRT) jijini Dar es Salaam, Awamu ya Pili, Tatu na Nne;
(vii) Daraja jipya la Sealander kutoka eneo la Coco Beach hadi Sea View Dar es Salaam na Daraja la Kigongo - Busisi mkoani Mwanza;
(viii) Mitambo ya kufua umeme ya Kinyerezi;
(ix) Viwanja vya ndege katika Mikoa mbalimbali kama vile Mtwara, Sumbawanga, Shinyanga, Musoma, Dodoma, Iringa na Songea;
(x) Barabara za Kitaifa, Mikoa na Vijijini katika mikoa mbalimbali nchini;
(xi) Majengo ya ofisi, makazi na huduma nyingine katika Makao Makuu ya Serikali – Dodoma; na
(xii) Ujenzi na uendeshaji wa viwanda mbalimbali nchini.

Hii ni baadhi tu ya miradi kwani ni dhahiri kuwa ipo/itakuwepo, miradi mingine mingi katika Sekta Binafsi na ya Umma itakayotoa fursa zaidi za ajira, na kuongeza ujuzi kwa

Wahandisi na Wataalam wengine wa Kitanzania, hivyo hatimaye kuchangia katika maendeleo ya taifa.

**Ndugu wa Wahandisi, Mabibi na Mabwana;**

Pamoja na kuwepo kwa fursa mbalimbali kama nilivyozitaja, jambo ambalo ninapenda kulisisitiza kwenu ni suala la kuwepo kwa **utayari** wenu (*readiness*) na **uwezo** wenu (*capacity*) katika kuzifikia na kufaidika na fursa hizi. Nafarijika sana na jitihada za Bodi ya Usajili wa Wahandisi, Taasisi mbalimbali za elimu nchini na wadau wengine za kuwaendeleza Wahandisi na wataalam wa fani zinazoendana na Uhandisi, ili kuwajengea **utayari** na **uwezo** wa kuwania fursa mbalimbali za ujenzi wa uchumi wa viwanda. Mfano mmojawapo wa jitihada hizi ni mafunzo kwa vitendo ambayo Bodi ya Usajili wa Wahandisi inayatoa kwa Wahandisi Wahitimu. (*Structured Engineers Apprenticeship Programme* (SEAP)).

Mpango huu umewasaidia vijana wengi kupata mafunzo kwa vitendo, uzoefu na hatimaye kusajiliwa kama Wahandisi Wataalam (*Professional Engineers*) kwa mujibu wa Sheria ya Usajili wa Wahandisi. Nimejulishwa kuwa hadi kufikia mwezi Juni, 2017, tayari Wahandisi Wihitimu 4,264 wameshafaidika na mpango huu, na kati yao Wahandisi 2,386 wameshahitimu. Leo tumeshuhudia baadhi ya wahitimu hao wakila kiapo na kusajiliwa kama Wahandisi Wataalam. Aidha, Serikali kupitia Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano itaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kufanikisha mafunzo haya kwa Wahandisi Wahitimu ambao idadi yao inazidi kuongezeka. Napenda kuishukuru Serikali ya Norway kwa msaada wake katika kufanikisha mafunzo haya kwa Wahandisi Wahitimu wanawake. Aidha, naishukuru pia Benki ya Dunia kwa kukubali kutenga fedha kupitia mradi wa "*Dar es Salaam Urban Transport Improvement Project*" kwa ajili ya mpango huu.

Aidha, kutokana na mahitaji makubwa ya mafundi sanifu kwenye uendelezaji wa viwanda, Serikali kupitia Bodi ya Mikopo kwa Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB) itatenga fedha kwa ajili ya kusomesha wataalam hawa kwa kiwango cha Stashahada (Diploma) kwenye vyuo vya Dar es Salaam Institute of Technology (DIT), Mbeya *University of Science and Technology* (MUST), *Arusha Technical College* (ATC), *National Institute of Transport* (NIT), Chuo cha Maji, na vyuo vingine vinavyostahili.

Hali kadhalika, naipongeza Bodi ya Usajili wa Wahandisi kwa kusimamia utolewaji wa mafunzo ya kuendeleza taalum ya kihandisi (*Continuing Professessional Development* – CPD) yanayotolewa na Chama cha Wahandisi Washauri Tanzania (*Association of Consulting Engineers Tanzania* – ACET) na Taasisi ya Wahandisi Tanzania (*Institution of Engineers Tanzania* – IET) yenye lengo la kuhakikisha Wahandisi wanaendana na mabadiliko ya kisayansi na kiteknolojia katika utekelezaji wa majukumu yao. Ni muhimu Wahandisi tuelewe kuwa kila wakati Teknolojia mbalimbali duniani zinaendelea kubadilika, hivyo ni lazima kuendelea kujifunza ili kukuza na kuboresha utaalamu wetu. Vinginevyo tutaachwa nyuma na kushindwa kufanikiwa katika soko la ushindani.

**Ndugu Wajumbe wa Mkutano, Mabibi na Mabwana:**

Serikali kwa ujumla inatambua umuhimu na kuthamini Taaluma ya Wahandisi katika kufanikisha miradi na shughuli mbalimbali za Serikali. Nafarijika kuona kuwa TAMISEMI ambako ipo miradi mingi inayowagusa wananchi moja kwa moja imeendelea kutambua umuhimu wa Wahandisi na inawatumia katika miradi ya ujenzi katika Halmashauri zake. Kufuatia uamuzi huo, idadi ya Wahandisi wanaotumika katika miradi hiyo imeongezeka kutoka 129 mwaka 2003 hadi kufikia 586 mwaka 2017. Naamini TAMISEMI itaendelea kuwatumia kikamilifu Wahandisi katika shughuli za Wakala mpya wa Barabara za Vijijini na Mijini (*Tanzania Rural and Urban Roads Agency* - TARURA), ulioanzishwa katika mwaka huu wa fedha 2017/2018.

Hata hivyo, napenda kuikumbusha Bodi ya Usajili wa Wahandisi kuhusu umuhimu wa kutekeleza kikamilifu mamlaka yake ya kisheria ya kuhakikisha kuwa taaluma ya Uhandisi inalindwa ipasavyo kwa **kuiendeleza** na **kuidhibiti** ili ifanyike kwa **utaalamu** unaostahili, **weledi** na kwa kuzingatia **maadili** yaliyowekwa kisheria. Sisi sote ni mashahidi wa baadhi ya barabara, madaraja, majengo n.k., ambayo yameharibika ndani ya muda mfupi sana tangu kujengwa na kusababisha hasara kubwa kwa Serikali na nchi kwa ujumla. Napenda kusisitiza umuhimu wa ERB pamoja na Bodi nyingine za Kitaaluma kuchukua hatua kali kwa wahusika wote, ambao wanaidhalilisha taaluma yao kwa kufanya kazi chini ya viwango.

Kwa upande mwingine, Serikali itatumia vyombo vyake mbalimbali ili kufuatilia wote wanaohusika katika utoaji wa Zabuni kwa Makampuni ambayo yanashindwa kutekeleza kwa ufanisi miradi wanayopewa, ili kubaini endapo kuna mapungufu ya kiutendaji ama mazingira ya rushwa katika utoaji wa Zabuni kwa Makampuni husika, na hivyo kuchukua hatua kali kwa wote watakaobainika kukiuka taratibu.

**Ndugu wa Wahandisi, Mabibi na Mabwana;**

Ushirikiano baina ya Sekta Binafsi na Sekta ya Umma katika ujenzi wa uchumi wa Viwanda ni jambo linalotiliwa mkazo na Serikali ya Awamu ya Tano. Serikali inatambua kuwa viwanda vitajengwa na wawekezaji kutoka Sekta Binafsi kutoka ndani na nje ya nchi, hivyo inafanya kila jitihada kuweka mazingira mazuri na vivutio mbalimbali kwa ajili ya uwekezaji wenye tija kwa wawekezaji. Baadhi ya mazingira hayo ni:

(i) Uwepo wa rasilimali watu iliyoandaliwa vyema kwa ajili ya ujenzi na uendeshaji wa viwanda;
(ii) Uwepo wa malighafi za kilimo, ngozi, misitu, madini na nyinginezo zinazovunwa nchini kwa ajili ya viwanda hivyo;
(iii) Ujenzi wa miundombinu ya kisasa kama vile barabara, reli, bandari, umeme, maji n.k., ambayo itarahisisha upelekaji wa malighafi viwandani, na usafirishaji wa bidhaa kutoka viwandani kwenda sokoni na kwa walaji, pamoja na matumizi mengine; na
(iv) Kuwepo kwa fursa za viwanda ambavyo vimerejeshwa Serikalini kutokana na wawekezaji wa awali kutoviendeleza.

Hali kadhalika Serikali inahimiza ushirikiano miongoni mwa Wizara, Idara na Taasisi za Serikali katika ujenzi na uendeshaji wa viwanda kwa lengo la kufanikisha azma ya Tanzania ya Viwanda. Kwa mfano, ushirikiano baina ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano na Wizara nyingine, hususan Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI); Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji; na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na kadhalika, ni muhimu sana katika kufanikisha azma hiyo. **Hivyo rai yangu kubwa kwenu ni kwa wadau wote kutoka Sekta Binafsi na ya Umma kudumisha ushirikiano katika kufanikisha ujenzi wa Tanzania ya viwanda**.

**Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa, Mheshimiwa Mwenyekiti wa Bodi, Ndugu Wahandisi, Wageni Waalikwa, Mabibi na Mabwana;**

Nihitimishe hotuba yangu kwa kuwatakia Mkutano mwema na majadiliano yenye tija. Ni matarajio yangu kuwa mapendekezo mtakayoyatoa katika Mkutano huu yatawasilishwa katika vyombo husika Serikalini kwa ajili ya kuyafanyiwa kazi. Baada ya kusema hayo, ninayo furaha sasa kutamka kwamba **Maadhimisho ya Siku ya Wahandisi kwa Mwaka 2017 yamefunguliwa rasmi**.

**Mungu Ibariki Tanzania,**
**Mungu Wabariki Wahandisi wa Tanzania,**
**Asanteni kwa Kunisikiliza.**